

Kufanya usafi

 Espen Stranger-Johannessen

 Aakanee

 Jacob Haule

 2

 Kiswahili SW



Kwanza, anafagia sakafu kwa kutumia ufagio.



Kisha anasafisha kwa kifyonza vumbi.
Kifyonza vumbi kinafanya kazi vizuri.



Kisha anachukua ndoo ya maji na deki.



Anadeki sakafu.



Anatupa takataka kwenye pipa la taka na anaweka mfuko mpya ndani yake.



Anatupa takataka nje.




Anahitaji glavu, sponji na kiowevu cha kusafishia.




Anasugua eneo chafu sakafuni kwa kutumia sponji na kiowevu cha kusafishia.



Kisha anasafisha dirisha.



Sebule yake haiko sawa kabisa.



Anapanga vitu juu. Sasa iko vizuri na safi.



LIDA Stories

lidastories.net

Kufanya usafi

 Espen Stranger-Johannessen

 Aakanee

 Jacob Haule

